TAMKO LA KONGAMANO LA KITAIFA LA

MTANDAO WA WANAWAKE, KATIBA, UCHAGUZI NA UONGOZI

VIWANJA VYA TGNP, MABIBO

MEI 20-21, 2024

AJENDA YA MWANAMKE; TURUFU YA USHINDI

UTANGULIZI:

Mtandao wa Wanawake, Katiba, Uongozi, na Uchaguzi ulianzishwa kwa madhumuni ya kushinikiza mchakato wa katiba mpya yenye mrengo wa jinsia kwa kujumuisha sauti za wapenda haki nchini kwa dhamira ya kuhoji na kubomoa mifumo kandamizi ukiwemo mfumo dume. Mtandao huu ulianza kama Mtandao wa Wanawake na Katiba na ulihusisha asasi za kiraia zaidi ya 65 mwaka 2011 na ulitokana na vuguvugu la tapo lililojikita katika kuhakikisha kuwa mchakato na maudhui ya Katiba ulionzishwa katika awamu ya nne ya Mh. Jakaya Kikwete, unajumuisha sauti za wanawake na wasichana hasa walio pembezoni. Mtandao huu ni mwendelezo wa kupigania haki na ajenda ya ukombozi wa wanawake wa kimapinduzi.

Katika kuendeleza ajenda ya Katiba yenye mrengo wa jinsia, Mtandao uliandaa kongamano la kitaifa Mei 20-21, mjini Dar es Salaam ililojumuisha wanamtandao zaidi ya 200 kutafakari na kupanga mikakati ya ushiriki mpana na wenye tija kwa wanawake kuendelea kuongoza harakati za kuchagiza demokrasia shirikishi.

Katika muktadha wa sasa Mtandao umebainisha kuendelea kuwepo na vikwazo vingi na vizuizi vingi na upotoshaji wa kudai haki za wanawake hasa tunapokaribia wakati huu wa uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi wa Rais mwakani. Kwa mfano, kupuuzwa kwa madai ya kuingiza vipengele ambavyo vingetoa nafasi sawa za ushiriki wa wanawake katika mchakato mzima wa uchaguzi ikijuimuisha wagombea, wapiga kura na washiriki ndani ya vyama vya vyote vya siasa. Hali hii inaondoa matumaini ya ushiriki wa wanawake katika uchaguzi wa ngazi zote.

Uchambuzi yakinifu wa mtandao ulibaini mapungufu makubwa katika taratibu na kanuni za uchaguzi ikiwa ni pamoja na uwazi na uchelewashwaji wa hizo kanuni. Kwa mfano hadi sasa taratibu za uchaguzi wa serikali za mitaa haujafikia wananchi, hali ambayo ina uwezo

wa kuchangia kufifisha jitihada za kuelimisha wananchi na kuwaandaa ushiriki wa wanawake katika mchakato wa uchaguzi.

Wanamtandao wa Wanawake, Katiba, Uongozi na Uchaguzi UNALAANI vikali na KUKEMEA:

Kauli za viongozi zinazokinzana aidha kwa makusudi au kwa kutokuwa na uelewa wa kutosha juu ya ajenda ya Ukombozi wa Wanawake Kimapinduzi.Kauli hizi zinaleta taharuki na kushusha harakati za kudai haki sawa kwa wanawake na wasichana nchini hasa kipindi hiki tunapolekea uchaguzi wa serikali za Mtaa na baadade uchaguzi mkuu hapo mwakani.

WANAMTANDAO TUNADAI YAFUATAYO;

1. Vyombo vyote vinavyohusika na uchaguzi na usalama wakati wa uchaguzi vitoe mazingira wezeshi, ili wanawake wote waweze kushiriki. Kadhalika, vyombo vinavyosimamia uchaguzi na utoaji wa haki, viweze kuweka mazingira wezeshi na kusimamia haki katika ngazi zote na ulinzi .
2. Kanuni na taratibu za kuongoza uchaguzi wa serikali za mitaa, uwe wazi, shirikishi na ujumuishe masuala ya jinsia ikiwamo makundi ya watu wenye ulemavu.
3. Ufuatiliaji wa vikwazo vinavyojitokeza katika ngazi za uchaguzi kwa mfano (uteuzi
4. Vyama vya siasa vihakikishe teuzi za watia nia na wagombea vinazingatia misingi ya usawa wa jinsia na kutoa ulinzi wa kuondoa vikwazo vyote vya ukatili.
5. Vilevile tunadai vyama vya siasa vihakikishe wagombea wanapata ulinzi dhidi ya vitendo vya ukatili.
6. Vyama vya siasa vihakikishe na kuwajibishwa kuhusu ugawaji na matumizi ya rasilimali za uchaguzi yanayojenga ulingano kati ya wagombea wa kike na wa kiume ndani ya vyama.
7. Wagombea wote, wakiwamo wa kiume watabeba ajenda inayotetea haki jumuishi ikiwamo za wanawake na Watoto. Mtandao umeandaa ajenda yake kwa kutumia ilani ya uchaguzi , ikitarajia ilani hiyo iangaliwe na kufanywa kuwa sehemu ya ajenda ya kampeni zao.
8. Tunavitaka vyombo vya Habari na jamii vishiriki kikamilifu katika mijadala endelevu na ya usawa wa kijinsia, kadhalika kuendelea kukemea kauli na taarifa za upotoshwaji zinazorudisha nyuma ajenda ya mwanamke na uongozi.

HITIMISHO:

Washiriki wa Kongamano hili la kitaifa la Mtandao wa Wanawake, Katiba, Uongozi na Uchaguzi, lililobeba kauli mbiu ya Mtandao: **Ajenda ya Mwanamke; Turufu ya Ushindi**

wanaamini kwamba uchaguzi ujao wa uongozi wa ngazi ya chini hadi ya kitaifa utakuwa ni huru na shirikishi. Mtandao utaendelea kueneza elimu juu ya umuhimu wa katiba yenye mrengo wa jinsia, ushiriki wa wanawake katika uchaguzi na uongozi, ikiwa ni pamoja na kujiimarisha kiteknolojia katika utoaji taarifa kwa wakati katika kupambana na sauti zenye mwelekeo wa kutugawa na kudhoofisha nguvu zetu za pamoja kuvunja mifumo kandamizi. Tunaahidi kuendelea kushinikiza vyama vya kisiasa kutekeleza sera za jinsia na kufuatilia kwa karibu magaeuzi yoyote yanayokinzana na ajenda yetu. Mtandao pia utaendelea kufuatilia na kupaza sauti kuhakikisha mageuzi chanya ya sheria mbali mbali, ikiwa ni pamoja na yale ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi yanatekelezwa. Pia Mtandao utaendelea kujijiimarisha katika kukuza hamasa na kujenga uwezo wa wanawake kushiriki na kugombea nafasi mbali mbali za kisiasa.